

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA HAMSINI NA SABA**

**23 JUNI, 2021**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA HAMSINI NA SABA – TAREHE 23 JUNI, 2021

#### I. DUA:

#### II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

##### WAZIRI MKUU:

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevywa ya Mwaka 2020.

##### WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2021 (*The Finance Bill, 2021*).

##### MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Maoni ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2021 (*The Finance Bill, 2021*).

### III. MASWALI:

#### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

#### 475. MHESHIMIWA FESTO RICHARD SANGA (MAKETE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya cha Ikuwo Wilayani Makete.

#### 476. MHESHIMIWA MIRAJI JUMANNE MTATURU (SINGIDA MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga Vituo vya Afya vya Issuna, Ikungi, Makungu, Ntuntu na Misughaa ili kurahisisha huduma za dharura Wilayani Ikungi kwa kuwa Wilaya hii inapitiwa na Barabara ya Dodoma – Mwanza ambayo imekuwa na ajali za mara kwa mara;

(b) Je, ni lini Serikali itapeleka Gari la Wagonjwa ili kuwahisha Majeruhi na Wagonjwa katika Hospitali za Rufaa.

**477. MHESHIMIWA DKT. CHARLES STEPHEN KIMEI (VUNJO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali inaweza kuwahakikishia Wananchi wa Moshi Vijijini kuwa barabara za Himo – Kilema, Pofu – Mandaka, Uchira – Kisomachi na Mabogini – Kahe - Chekereni zitawekwa kwenye Bajeti ya Mwaka 2021/2022 ambayo pia ni ahadi ya Mheshimiwa Rais.

**478. MHESHIMIWA DKT. ALICE KARUNGI KAIJAGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali imejipangaje kutatua changamoto iliyopo katika Vituo vya kutolea huduma za Afya ya kukosekana kwa Idara ya Huduma ya Mazoezi Tiba na Utengamao ukilinganisha na ongezeko la Wagonjwa wanaohitaji aina hiyo ya tiba.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**479. MHESHIMIWA ENG. EZRA JOHN CHIWELESA (BIHARAMULO MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, ni lini Serikali itanza Ujenzi wa Soko la kimkakati la Rusahunga Wilayani Biharamulo litakaloharimu Shilingi Bilioni 3.5 kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri Mkuu Bungeni.

**WIZARA YA MAJI:**

**480. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINA CHRISTOPHER MNZAVA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itapeleka huduma ya Maji safi na salama kwa Wananchi wa Kata za Mwamala, Samuye, Busanda, Usule, Bukene na Imesela.

**WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

**481. MHESHIMIWA DUNSTAN LUKA KITANDULA (MKINGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, ni lini Wananchi wa Kata ya Mwakijembe ambao mashamba yao yalitwaliwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) watalipwa fidia.

**WIZARA YA NISHATI:**

**482. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itamaliza ujenzi wa Umeme wa *Grid* ya Taifa Mkoani Katavi.

**WIZARA YA KILIMO:**

**483. MHESHIMIWA DANIEL AWACK TLEMAI  
(KARATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina Mkakati gani wa kuendeleza Mashamba ya Karatu – Bendhu pamoja na kuwalipa Wafanyakazi wa Mashamba hayo.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**484. MHESHIMIWA MAIMUNA SALUM MTANDA  
(NEWALA VIJINI):**


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Mkwiti – Amkeni inayounganisha Mkoa wa Lindi na Mtwara kupitia Mtama.

#### **IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:**

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2021 (*The Finance Bill, 2021*).



**DODOMA  
23 JUNI, 2021**



**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**